# BASI KUMBUKA NI WAPI ULIKOANGUKA UKATUBU

## MAANDIKO: UFUN. 2: 1-5, Ezek. 16: 1 – 16

1. **UTANGULIZI:**

Katika maisha haya, nimejifunza sana kwamba binadamu ana kawaida ya kufurahia kitu anapokipata kwa mara ya kwanza; anakuwa haoni kasoro yoyote ile maana moyo wake wote anauwekeza pale.

***Mfano***: Mtu kama hana kazi baada ya kupata elimu yake au hata kama hana elimu, muda wake wote anakuwa anatamani apate kazi ya aina yoyote, na anapoipata, mwanzoni ataifanya kwa kuifurahia na kwa bidii zake zote, lakini polepole kwa kadri atakavyoizoea na kupata kipato, baadaye anaanza kuidharau na kuanza kutafuta kazi iliyo bora kuliko ile!!! Au wakati vijana wawili wanakubaliana **KUOANA,** ukiipasua mioyo yao jinsi kila mmoja anavyomfurahia mwenzake utashangaa, hakuna anayeona kasoro ya aina yoyote kwa mwenzake kwa sababu moyo wake wote anauweka pale; lakini waangalie baada ya muda Fulani; tayari wameanza kukosoana, na wakati mwingine hata kuanza kujuta kwa nini niliolewa/nilioa huyu; anafikiri angeoa/angeolewa na Fulani angekuwa na maisha Bora zaidi!!! **Hii ndiyo kawaida kabisa ya kila binadamu ambaye hajapata neema hasa ya wokovu halisi!!!**

- Hali hii ndiyo Mungu anayozungumza na Taifa la Israeli!! Mungu alilikuta Taifa hili likiwa katika hali mbaya sana, ni yeye aliyelitoa katika hali hii mbaya kwa mkono wake wa nguvu na kulibariki na kuwapo utukufu mwingi na heshima na utisho usio wa kawaida!! Lakini baadaye Israeli walisahau kabisa Mungu alikowatoa na kuanza kuutumainia uzuri (Baraka) na kumsahau Mungu kabisa. ***Ezek.16: 15 -34, 35-43.*** Kwa kweli kusahau alikotukuta Yesu na kututoa huko na kisha kutufikisha hapa tuliko sasa ni jambo la kutisha sana**.**

2. Angalizo hili la **kukumbuka** wapi Yesu alikotutoa Mtume Yohana anapewa ili aliambie Kanisa la Efeso ambalo Mtume Paulo alilianzisha kwa mateso mengi, na wengi wao walikuwa wanaabudu miungu. ***Mdo. 19: 8 – 12, 17 – 20, 23- 28***, ishara nyingi zilifanyika katika Efeso kuliko kawaida, na Kanisa la Efeso likawa kama makao Makuu ya Makanisa yote yaliyoanzishwa katika Asia kwa wakati ule, lakini polepole upendo wao kwa Mungu ukaanza kupoa!! Wakaanza kuridhia tena ibada ya kipagani na kushirikiana nao!! ***Ufun. 2: 1 - 5***

- **NDIVYO ILIVYO KWA KANISA LA LEO, WATEULE WENGI WAMEACHA KUFURAHIA WOKOVU WAO WA KWANZA NA KUTUNZA UTAKATIFU KWA GHARAMA ZOZOTE KAMA WALIVYOKUWA WAKIFANYA MWANZO WA KUOKOKA KWAO; NA SASA WAMEANZA KUZUBAISHWA NA BARAKA AMBAZO MUNGU AMEWAPA WAKIWA NDANI YA WOKOVU!! Ebr. 10: 32 – 38!!!** Hili ni jambo la hatari sana tena sana ***– 2Nyakt. 16: 1 – 14.***

**Note**: **Kwa mteule yeyote aliye makini, Baraka za Mungu wake kamwe haziwezi kumbadilisha moyo wake halisi na tabia yake ya kumcha Mungu, na badala yake zitamchochea kumpenda Mungu zaidi pamoja na kumtafuta zaidi – Mfano wa Yusufu. Mwz. 45: 4 – 14, au Daniel – Dan. 6: 4 – 10, au Daudi – 2Samwl. 7: 1 – 2 n.k.**

3. Mara nyingi sana adui anapiga vita tusikumbuke Yesu alitutoa wapi ili **atuburute** baadaye; wana wa Israel walitakiwa kamwe wasisahau jinsi Mungu alivyowapenda na kisha akawatoa katika mikono ya Farao kwa mkono wake wenye nguvu***- Kut. 11: 1, 12: 29 – 42, Kut. 14: 15 - 31,*** **Hata kule kulishwa kwa Mana na Kware, kwa miaka 40 kila siku bila wao kulima, au kuishi miaka 40 bila kwenda Hospital kutibiwa, au miaka 40 bila nguo zao kuchanika n.k. hawakupaswa kunung'unika wala kusahau matendo kama haya, lakini wakasahau!!!** ***Kumb. 8:1-18.***

(Tangu Adamu, hakuna binadamu aliyekuwa anakula bure bila kufanya kazi; ni Taifa la Israeli pekee ambao ulipokuwa unafika wakati wa kula, mana inadondoka, kware nao wanadondoka, wanaokota na kupika na kula, tena wakapewa na masharti ya kutokula kiporo!! ***Kut. 16: 10 - 18***

***Note:*** **Siri pekee iliyowasaidia wateule wengi kutosahau Yesu alikowatoa ni hii "hawakujipima Baraka zao kutokana na vitu walivyonavyo kama fedha nyumba, magari, dhahabu, elimu n.k. bali walijipima kwamba wamebarikiwa sana na Bwana pindi walipoona siku kwa siku wanaendelea kumtii Mungu na Neno lake pamoja na kumpa heshima yake kama Baba yao anayewawazia mema daima" Yer. 29:11, Isay. 66:1-2**

***NB***:Kumbuka jambo hili daima katika maisha yako/yangu ya wokovu kama unataka upendo wako wa kwanza kwa Bwana Yesu/kwa mwezi wako usichuje daima.

a. **Kuwa na saburi (kuvumilia) wakati unapojikuta unapita katika dhiki Fulani kwa sababu ya kumpenda Yesu/mwezi wako (saburi ndiyo kinga kabambe ya kukufanya usisahau ulikotoka na mwenzi wako/Bwana Yesu. *Ebr. 10: 36, Luk. 21:19* mfano wa mkulima – *Yak. 5: 7 – 8.***
b. Weka moyo wako wote (macho) kwenye furaha kuu iliyo mbele yako (***Ebr. 12: 1-3)*** na kudharau mambo ya muda unayoyapitia kwa kitambo tu!!! Mwanamke angeangallia utungu anaoupata saa ya kuzaliwa mwana, asingekubali kuzaa tena; daima huweka moyo wake wote kwenye furaha ya mbeleni!!! ***Yoh. 16: 20 – 22.*** Nasi tumeahidiwa mji wa ajabu mno na Bwana, ***Ufun. 21 yote;*** leo tukubaliane na **Nabii Isaya kwa kusema "Na hapo patakuwa na njia kuu na njia, nayo itaitwa, njia ya utakatifu, wasio safi hawatapita juu yake, bali itakuwa kwa ajili ya watu hao (watakatifu) wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo. *Isay.35:8. Amina*.**

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***12/06/2022***